JINA LA MWANAFUNZI …… JINA LA SHULE ……

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA KILIMANJARO

MTIHANI WA MHULA WA II – DARASA LA TANO

06

URAIA NA MAADILI

Muda: Saa 1:30
Novemba 2024

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali sita (6).
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.
3. Andika majibu yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika kila swali.
4. Andika majibu yote kwa kutumia kalamu ya **bluu** au **nyeusi**.
5. Andika jina lako na jina la shule kwenye nafasi ilioachwa wazi juu ya karatasi.

KWAMATUMIZI YA MTAHINI TU		
NAMBA YA SWALI	ALAMA	SAINI YA MTAHINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		

SEHEMU A. (ALAMA 20)

1. Chagua jibu sahihi kati ya majibu uliyopewa na uandike herufi yake.

JINA LA MWANAFUNZI …… JINA LA SHULE ……

i. Bwana Chapakazi ni mtaalamu wa mambo ya kisheria, ambaye anatoa msaada wa kisheria kwa mtu binafsi anapopatwa na changamoto za kisheria. Bwana Chapakazi tutamtumiaje?
(A) Hakimu
(B) Jaji
(C)Mshauri
(D) Wakili
(E) Mkaguzi

ii. Uharibifu wa ardhi kwa Tanzania husababishwa na kazi za kibinadamu. Ni kazi zipi kati ya zifuatazo husababisha uharibifu wa ardhi?
(A)kutumia mbolea
(B)kupanda miti
(C)ufugaji ulipitiliza
(D)kilimo cha matuta
(E)kutandaza

iii. Kiuhalisia wananchi wote hawawezi kuhudhuria kwenye mkutano wa wilaya, badala yake wanachagua watu wachache wa kuwawakilisha kwenye mkutano . Je hao wawakilishi wataitwaje?
(A)wakuu wa wilaya
(B)wenyeviti wa wilaya
(C)wenyeviti wa vijiji
(D)madiwani
(E)watendaji Kata

iv. Mzai na rafiki yake Timbulo waliona gari lililobeba majeruhi likiwa na mwendo mkali kuelekea hospitali ya Taifa. Unafikiri Mzao na rafiki yake waliona nini? { }
(A)jeshi la zimamoto
(B)gari la polisi
(C)lori la moto
(D)gari la wagonjwa
(E)basi la abiri

v. Bwana Jakobo alituhumiwa kwa kesi ya mauwaji na wizi wa silaha ni mahakama ipi kati ya zifuatazo inahusika na kujadili kesi ya bwana Jakobo
(A)mahakama ya mwanzo
(B)mahakama kuu
(C)mahakama ya wilaya
(D)mahakama ya hakimu mkazi
(E)Mahakamaya rufaa

vi. Mwande alikataa kujifunza pamoja na Mwagu kwa sababu Mwagu ni mlemavu wa ngozi (albino). Tabia aliyoonyesha Mwande inaitwa.
(A)uvumilivu
(B)unyanyapaa
(C)ukandamizaji wa kijinsia
(D)uonevu
(E)Unyanyasaji wa kijinsia

vii. Chikunde alimjulisha rafiki yake Zuena kuhusu ugomvi wa wazazi wake uliotokea nyumbani ila akamwomba asimwambie mtu mwengine.Kwa bahati mbaya Zuena alianza kusambaza Habari hiyo kwa wanafunzi wengine shuleni.Tabia iliyooneshwa na Zuena inaitwa

(A)usaliti
(B)kulipa kisasi
(C)unafiki
(D)uaminifu
(E)Ustahimilivu

viii. Bakari alizaliwa mwaka 1997.Je atakuwa ameshiriki jumla ya chaguzi kuu ngapi Tanzania?
(A)sita
(B)tatu
(C)mbili
(D)nne
(E)tano

ix. Kamazigawa ni kiongozi katika eneo la utawala ambalo ni kubwa kuliko kata na dogo kuliko wilaya.Je Kamazigawa ni nani? { }
(A)diwani
(B)mkuu wa mkoa
(C)afisa mtendaji kata
(D)Mkuu wa wilaya
(E)Afisa Tarafa

JINA LA MWANAFUNZI …… JINA LA SHULE ……

x. Mavunde ni meneja wa rasilimali watu katika kampuni ambapo ameajiri ndugu na rafiki zake wengi na kampuni haifanyi vizuri .Kitendo kilichofanywa na Mavunde kinaitwa { }

(A)Ushirika
(B)uchapakazi
(C)mshikamano
(D)upendeleo
(E)Utandawazi

2. Oanisha maneno kutoka katika kifungu A na yale ya kifungu B

KIFUNGU A	MAJIBU	KIFUNGU B
i. Mwaka mpya		A. Tarehe 1 mwezi wa Tano kila mwaka
ii. Siku ya wafanyakazi		B. Tarehe 7 mwezi wa nne kila mwaka
iii. Mapinduzi ya Zanzibar		C. Tarehe 1 mwezi wa kwanza kila mwaka
iv. Siku ya Karume		D. Tarehe 12 mwezi wa kwanza kila mwaka
v. Siku ya Nyerere		E. Tarehe 26 mwezi wa nne kila mwaka
		F. Tarehe 9 Desemba kila mwaka
		G. Tarehe 14 mwenzi wa kumi kila mwaka

3. Tumia maneno yaliyo kwenye kisanduku kujaza nafasi zilizo achwa wazi.

Diwani, Afisa kilimo kata, Afisa Mtendaji wa kijiji, Afisa maendeleo kata, Afisa Elimu kata, Diwani wa viti maalumu, Afisa afya kata, Afisa Mtendaji kata

i. Msimamizi wa shughuli zote za kiserikali katika kata ni _____
ii. Muwakilishi wa wananchi wote katika kata ni _____
iii. Msimamizi wa shughuli zote za elimu katika kata ni _____
iv. Huteuliwa na chama chake pia ni mjumbe wa kamati ya maendeleo ya kata _____
v. Husimamia shughuli mbali mbali za maendeleo katika kata pia huelimisha jamii kuhusu kutunza mila na desturi _____

SEHEMU B: (ALAMA 20)

4. Bainisha kauli zifuatazo kama ni tendo la '**uvumilivu**' au '**uaminifu**' kisha andika jibu kwenye nafasi uliyopewa kwenye kisanduku.

KITENDO	UVUMILIVU	UAMINIFU
i. Kuwa mtiifu na mkweli muda wote		
ii. Kuwataarifu watu wazima baada ya kuvunja sahani		
iii. Kumtafuta mwenye kalamu uliyoiokota		

JINA LA MWANAFUNZI …… JINA LA SHULE ……

iv.	Kuepuka maneno makali wakati chakula cha mchana kimechelewa		
v.	Kuwa mstahimilivu uwapo mgonjwa		

5. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika jibu sahihi

i. Ni nembo gani ya taifa inayotambulisha nguvu na mamlaka ya Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?_____

ii. Katibu wa baraza la madiwani wilaya ni _____

iii. Nani ni katibu wa kamati ya ushauri mkoa? _____

iv. Ni mhimili upi wa serikali unahusika na utungaji wa sheria za nchi?_____

v. Taja viongozi wakuu wawili wa kamati ya maendeleo ya Kata

(a) _____

(b) _____

SEHEMU C: (ALAMA 10)

6. Chunguza picha ifuatazo kisha jibu maswali



i. Ni shughuli gani inafanywa na wanafunzi kwenye picha hapo juu? _____

ii. Bainisha umuhimu wa kufanya shughuli hiyo kwenye kielelezo hapo juu

_____

iii. Nini kitatokea endapo shughuli inayofanywa katika picha haitafanyika?

_____

iv. Ni tabia gani inajengwa na wanafunzi kwa kushiriki katika shughuli za umma?

_____

v. Uwezo wa kufanya shughuli iliyooneshwa kwenye picha bila kusimamiwa huitwa

_____

JINA LA MWANAFUNZI …… JINA LA SHULE ……

MAJIBU

1.

i	ii	iii	iv	v	vi	vii	viii	Ix	x
D	C	D	D	B	B	A	C	E	D

2.

i	Ii	iii	iv	V
C	A	E	B	G

3 (i) Afisa Mtendaji kata/ Ward Executive officer
(ii) Diwani/ Ward councillor
(iii)Afisa Elimu kata/ Ward Education officer
(iv)Diwani wa viti maalumu/ Special Seat Ward councillor
(v)Afisa Maendeleo kata

4 (i)UAMINIFU
(ii) UAMINIFU
(iii) UAMINIFU
(iv) RESILIENCE

(v)RESILIENCE

5 (i)Bendera ya Raisi / Presidential flag

(ii)Mkurugenzi/ District Executive Director

(iii)Katibu Tawala Mkoa/ Regional Administrative Secretary

(iv)Bunge/ Parliament

(v)Diwani na afisa mtendaji kata/ Ward Councillor and Ward Executive Officer

7. (i) Usafi wa mazingira/environmental cleanliness

(ii) Utunzaji wa mazingira/ environmental conservation

(iii) kuenea kwa magonjwa/ spread of diseases

Kuwepo kwa wadudu hatarishi/ attraction of dangerous insects

(iv) Uzalendo/ patriotism

v) Nidhamu binafsi/ self-discipline